# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

# RIPOTI YA MAPENDEKEZO YA KUANZISHWA KWA JESHI LA UTALII ZANZIBAR

**RIPOTI NAMBA 7/2021**

**IME WASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**NOVEMBA, 2021**

**MHESHIMIWA HAROUN ALI SULEIMAN,**
**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**
**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,**
**MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,**
**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA MASOUD ALI MOHAMMED,**
**WAZIRI WA NCH, AFISI YA RAIS, TAWALA LA MIKOA NA IDARA MAALUM ,**
**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA LELA MOHAMMED MUSSA**
**WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE,**
**ZANZIBAR**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Namba 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inapenda kuwasilisha Ripoti hii kuhusu Mapendekezo ya Kuanzisha Sheria ya Jeshi la Utalii Zanzibar

**……………………**

**KHADIJA SHAMTE MZEE**

**MWENYEKITI**

**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR**

**08 Novemba, 2021.**

# MAKAMISHNA WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR



**BIBI. KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI**



**BW. MTORO ALMAS ALI**
**KAMISHNA**



**BW. ALI ALI HASSAN**
**KAMISHNA**



**DKT. ALI AHMED UKI**
**KAMISHNA**



**BW. SALUM MAULID SALUM**
**KAMISHNA**



**MHE. JAJI AZIZA IDDI SUWEID**
**KAMISHNA**



**BW MUSSA KOMBO BAKARI**
**KATIBU**

| | |
|---|---|
| Mhe Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti |
| Mhe Aziza Iddi Suwedi | Kamishna |
| Dkt. Ali Ahmed Uki | Kamishna |
| Ndg. Ali Ali Hassan | Kamishna |
| Nd. Salum Maulid Salum | Kamishna |
| Nd. Mtoro Almasi Ali | Kamishna |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu |

**WATAFITI**

| | |
|---|---|
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu wa Tume |
| Nd. Hannat Bakari Hamad | Mtafiti wa Sheria |
| Nd. Mariam Rashid Ali | Mtafiti wa Sheria |

Ofisi za Tume ya Kurekebisha Sheria zinapatikana
Vuga, Zanzibar-
P.O BOX 2539,
Simu +255 24 2231136,
Nukushi +255 24 2231137,
barua pepe info@lrcz.go.tz,
tovuti www.lrcz.go.tz

**VIFUNGU VYA UTANGULIZI**

**Makamishna wa Tume…………………………………………………………i**

**Sheria zilizotumika…………………………………………………………..iv**

**SURA YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**……………………………………………………………1

2.0 Historia ya Jeshi la Utalii…………………………………………………..1

3.0 Kiini cha tatizo……………………………………………………………..2

4.0 Lengo la Utafiti…………………………………………………………….3

5.0 Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2020……...3

6.0 Sera ya utalii Zanzibar 2017……………………………………………….3

7.0 Mpango Mkakati wa Kamisheni ya utalii 2015-2020………………………..4

8.0 Mtazamo wa Wananchi Zanzibar Kuhusu Ulinzi Na Usalama kwa watalii….4

9.0 Uzoefu wa Nchi nyengine Katika Ulinzi na Usalama kwa Watalii…………...5

9.1 Uzoefu wa Tanzania Bara…………………………………………………..5

9.2 Uzoefu wa Jeshi la Polisi la Utalii Kenya……………………………………6

9.3 Uzoefu kwa Nchi ya Uganda………………………………………………..7

9.4 Uzoefu wa Nchi ya Rwada………………………………………………….8

9.5 Uzoefu kwa Nchi ya Madagascar…………………………………………..8

9.6 Uzoefu kwa Nchi ya India…………………………………………………..9

10.0 Hitimish……………………………………………………………………12

11.0 Mapendekezo……………………………………………………………..10

11.1 Mapendekezo ya Kisheria…………………………………………………10

11.2 Mapendekezo ya Kimuundo………………………………………………10

11.3 Mapendekezo mengine……………………………………………………..11

**SHERIA ZILIZOTUMIKA**

Sheria ya Kukuza Utalii No. 9 ya mwaka 1991

Sheria ya Utalii Namba 6 ya mwaka 2009

Marekebisho ya Sheria ya Utalii Namba 7 ya mwaka 2012

Azimio la haki za Binadamu la mwaka 1948

Mpango Mkuu Mkakati wa kamisheni ya utalii yam waka 2002

Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi 2020

Sheria ya Jeshi la Polisi yam waka 2011

Uganda Tourism act Namba 2 ya mwaka 2008

**SERA**

Sera ya utalii Zanzibar yam waka 2017

Ser ya utalii Rwanda yam waka 2009

## KUANZISHWA KWA JESHI LA UTALII ZANZIBAR

### 1.0 Utangulizi

Kamisheni ya Utalii Zanzibar ilianzishwa kwa Sheria Nam. 9 ya mwaka 1991 kwa lengo la kuratibu, kusimamia, kuendeleza na kutangaza Sekta ya Utalii. Hata hivyo, muundo na uendeshaji wake umewahi kubadilika mara kadhaa kwa kupitia Sheria ya Utalii Nam. 6 ya mwaka 2009 na marekebisho ya Sheria hiyo.[1]

Kutokana na kukuwa kwa Sekta hii muhimu, marekebisho mengine yanahitajika likiwemo suala zima la kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watalii kwa madhumuni ya kukuza Sekta hii muhimu na kuwafanya watalii wanaotoka nchi mbalimbali kufika katika visiwa hivi vya Zanzibar kufurahia mapumziko yao.

### 2.0 Chimbuko la Jeshi la Utalii Zanzibar

Kamisheni ya Utalii baada ya kupokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wadau wa Utalii kuhusu matukio yasiyoridhisha dhidi ya watalii na mali zao, iliamua kuanzisha jeshi maalum lenye dhamana ya kusimamia ulinzi katika sekta ya utalii Zanzibar. Kwa kupitia Sheria ya Utalii Nam. 6 ya mwaka 2009 kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 11, jeshi hilo lilianzishwa na liliundwa kwa mchanganyiko wa askari kutoka sekta mbali mbali, kama vile askari polisi, jeshi la kujenga uchumi (JKU), kikosi cha kuzuia magendo (KMKM) wakishirikiana na watendaji wa Kamisheni ya Utalii.

Jeshi hili lilifanya kazi zake chini ya maagizo na maelekezo kutoka Kamisheni, huku Kamisheni hiyo ikikabiliwa na vikwazo mbali mbali katika usimamizi

[1] Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii Namba namba 7 ya mwaka 2012

wake ikiwemo changamoto kubwa ya fedha ya kukimu uendeshaji wa jeshi hilo. Miongoni mwa mahitaji ya jeshi hilo yaliyohitaji gharama za fedha ni pamoja na chakula kwa ajili ya jeshi hilo, gharama za usafiri, gharama za posho kwa ajili ya jeshi pale linapofanya kazi katika muda wa ziada, vifaa na mahitaji mengine muhimu.

Kufuatia vikwazo hivyo, Serikali iliamua kuondoa kifungu cha Sheria kilichoanzisha jeshi hilo kupitia marekebisho ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2012 kwa kuwa utekelezaji wake ulionekana kuwa ni mgumu.

Hata hivyo, kutokana na changamoto za usalama kwa watalii zinavyozidi kuongezeka, wazo la kuwepo kwa jeshi hilo linahitaji kuzingatiwa upya kwa kuwekewa miongozo mizuri ili jeshi hilo liweze kutekeleza jukumu la ulinzi kwa watalii kwa nia ya kupunguza matukio ya kihalifu dhidi ya watalii Zanzibar.

## 3.0 Kiini cha tatizo

Utaratibu wa usimamizi wa utalii kwa mujibu wa Sheria Nam. 6 ya mwaka 2009 kama ilivyorekebishwa kupitia Sheria Nam. 7 ya mwaka 2012, bado haujakidhi haja katika kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watalii wa ndani na wageni wanaofika nchini kwa lengo la kuja kufanya Utalii. Hivyo, maboresho ya Sheria hiyo, Kanuni na miongozo zaidi inahitajika ili kuweza kupunguza changamoto kubwa iliyojitokeza miaka ya karibuni hapa Zanzibar juu ya uhalifu kwa watalii na mali zao.

## 4.0 Lengo la utafiti

Lengo la Utafiti ni kuangalia kwa kiasi gani suala la ulinzi na usalama kwa watalii linawekewa misingi ya Kisheria kupitia Sheria ya Utalii Nam. 6/2009.

## 5.0 Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya uchaguzi ya mwaka 2020

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua thamani ya utalii katika mchango mkubwa wa maendeleo ya nchi na hivyo imeeleza kwamba, utalii ni sekta kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar katika kuchangia pato laTaifa, fedha za kigeni na kutoa fursa za ajira. Kwa kutambua kuwa Zanzibar ina vivutio vingi na vya kipekee vya utalii, mkazo mkubwa umewekwa katika ushirikishwaji wa jamii, kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kuongeza idadi ya watalii wa daraja la juu na watakaokaa kwa muda mrefu. Katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi wa mwaka 2020, Serikali itatekeleza mapendekezo ya ratiba ya matokeo kwa ustawi kwa *kuimarisha ulinzi kupitia kikosi maalum* na ushirikishwaji wananchi[2]

## 6.0 Sera ya Utalii Zanzibar 2017

Miongoni mwa malengo na mikakati mbali mbali iliyolezwa katika sera ya Utalii Zanzibar ni suala la ulinzi na usalama. Sera hii ilikuwa na lengo la kuunga mkono azimio la haki za Binaadamu[3] ambalo lilitoa haki ya kusafiri na kutembea kwa uhuru. Hivyo, kwa upande wa sekta ya utalii, jambo hili nalo ni muhimu sana kwani utalii ni chombo kinachohitaji ulinzi, usalama na ushirikiano wa hali ya juu. Utalii ni kituo ambacho hukutanisha watu mbali mbali kutoka mataifa mbali mbali yenye mila, silka na tamaduni tofauti.

Kwa mantiki hiyo, ni wakati muafaka sasa kuziboresha sheria na kanuni za utalii kwa kuzungumzia kwa kina suala la usalama na ulinzi na kutilia mkazo ***kuanzishwa jeshi maaalum*** la kusimamia watalii na mali zao.

[2] Ibara ya 153(L) Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020

[3] Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu la Mwaka 1948

## 7.0 Mpango Mkakati wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar 2015-2020 (Zanzibar Commission for Tourim Strategic Plan 2015-2020)

Mpango Mkakati wa Kamisheni ya Utalii ni kuifanya Zanzibar kupitia utalii kuongeza soko la Utalii na uchumi kwa kutoa ajira, kuondosha umaskini, kulinda mazingira na kutunza utamaduni. Zanzibar inatambulika kiulimwengu kuwa ni kituo na kivutio kizuri kwa watalii. Ili kufikia hatua nzuri, Mpango Mkakati umeweka malengo nane muhimu ya kutiliwa nguvu ili kufikia mafanikio.Miongoni mwa malengo hayo ni kuboresha ulinzi na usalama kwa watalii[4].

Ulinzi na usalama ni miongoni mwa mambo muhimu yanayozingatiwa na watalii kabla ya kuchagua sehemu za kwenda kufurahia mapumziko yao. Nchi yoyote isipodhibiti matukio ya kihalifu yanayotokezea dhidi ya watalii, inaweza kupelekea nchi hiyo kuonekana sio sehemu ya kuaminika kwa amani, utulivu na usalama kwa watalii. Zanzibar kama ilivyo kwa nchi nyengine, inapaswa kuzingatia suala hilo kwa umakini.

## 8.0 Mtazamo wa Wananchi Zanzibar Kuhusu Ulinzi na Usalama kwa Watalii

Zanzibar ni visiwa vya amani na utulivu jambo ambalo linaipatia sifa kubwa ulimwenguni kote. Hivyo, vitendo vya kihalifu ikiwemo unyanyasaji na uporaji kwa watalii ni jambo ambalo wananchi hawalifurahii. Wananchi kupitia wawakilishi wao katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar, walionesha hisia zao katika suala la ulinzi kwenye sekta ya utalii ambapo walikusudia kuzuia Bajeti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ya mwaka 2021/2022

[4] Strategic issue 4 " Safety and Security of Tourists

mpaka Waziri husika atakapotoa ufafanuzi na msimamo kuhusu usalama kwa watalii kutokana na kuongezeka kwa matukio ya kihalifu.[5]

Kufuatia kadhia hiyo, Waziri husika[6] alieleza kwamba Serikali imeamua kutengeneza mazingira rafiki kwa watalii wanaofika katika visiwa hivi vya Zanzibar, hasa suala la usalama na ulinzi kwa watalii.[7] Aidha, tarehe 2 Februari 2021, Serikali iliwahakikishia watalii wanaofika Zanzibar juu ya usalama wao na kuahidi kufanya “patrol” sehemu za vivutio vya utalii ikiwemo sehemu za pwani.[8]

## 9.0 Uzoefu wa Nchi nyengine katika Ulinzi na Usalama kwa Watalii

Kilio kuhusu usalama na ulinzi kwa watalii ni kitu kinachozungumziwa kwa sauti kubwa duniani kote. Nchi mbalimbali mbali zimeonesha kwa kiasi gani zimeweza kupunguza ongezeko la matukio ya kihalifu kwa watalii mara tu baada ya kuanzisha jeshi maalum la kusimamia usalama kwa watalii na mali zao. Ripoti hii inafafanua uzoefu wa nchi mbali mbali katika suala la ulinzi kwa watalii.

## 9.1 Uzoefu wa Tanzania Bara.

Kwa upande wa Tanzania Bara, ilionekana upo umuhimu wa kuanzisha kitengo maaalum ambacho kitasimama kama ni jeshi la Utalii. Jeshi la Polisi lilianzisha kitengo maalum cha kushughulikia usalama kwa watalii na wageni wengine wanaokuja kutembelea Tanzania[9]. Jeshi la Polisi Tanzania limeamua kuunda

[5] Mh. Issa Haji Ussi Gavu (CCM-Chwaka) na Mh. Nadir Abdul- Latif (CCM- Chaani) walitishia kupinga kupitishwa bajeti ya Wizara ya Utalii bila ya maelezo ya kutosha kuhusu mikakati ya Serikali kwa usalama wa Watalii.

[6] Mh. Leyla Mohammed Mussa- Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale

[7] Maelezo yanapatikakana katika ukurusa wa 65 katika kitabu cha bajeti kwa mwaka 2021-2022

[8] https://allafrica.com

[9] Maelezo ya kiongozi wa kusimamia kitengo hicho maalum ACP Maria J.Nzuki wakati wa ziara ya kutembelea Bodi ya Utalii Tanzania.

kitengo hicho ili kuhakikisha watalii wanaokuja Tanzania wanafurahia kwa kiwango kikubwa usalama kwa kipindi chote ambacho watakaa nchini.[10]

Wazo la kuanzishwa Jeshi la Utalii limezungumzwa na Waziri wa Mambo ya Ndani kwa wakati huo, Dr. Emanuel Nchimbi wakati akiwasilisha Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2013/2014 ambapo alieleza kwamba Serikali itaanzisha jeshi maalum kwa lengo la kusimamia usalama wa watalii na mali zao.[11]

Mpango Mkuu wa Utalii Tanzania[12] umeeleza kwamba kwa kipindi kikubwa sasa tokea kutokea kwa shambulio la Ugaidi la Marekani, suala la usalama limekuwa ni kipaumbele kwa nchi yetu kama zilivyo nchi nyengine duniani. Tanzania tunalazimika kutekeleza mfumo wa usalama ili kuhakikisha watalii na mali zao wako salama katika kipindi chote wanapokuwa nchini. Kufanikiwa kwa dhamira hii ni kufungua ukuaji wa utalii kwa miaka mingi ijayo.

## 9.2 Uzoefu wa Jeshi la Polisi la Utalii Kenya

Miongoni mwa nchi ambazo zimeweka utaratibu wa ulinzi katika sekta ya utalii ni nchi ya Kenya. Kenya imeanzisha kitengo maalum kinachojulikana kama *“Tourist Police Unit”*.Kitengo hiki kimeanzishwa kisheria[13] kwa malengo yafuatayo:-

(a) Kulinda maisha ya watalii na mali zao

(b) Kutoa ulinzi na usalama kwa watalii

[10] Ibid, Dr. Nzuki alisema kwamba Jeshila Polisi nguvu zake zinaweza kupelekea faida kubwa katika maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini

[11] Tanzaniatourism.go.tz./en/ighlights/view/ police-force-etblishes-diplomatic –and-tourism-unit

[12] Tourism Master Plan strategy and Action Plan April, 2002

[13] Sec.24 National Police Service Act, 2011

(c) Kupokea na kufanyia kazi changamoto zote zinazowahusu watalii

(d) Kuchunguza makosa ya jinai yanayowahusu watalii na kuwafungulia mashtaka

(e) Kutembelea sehemu za fukwe, hoteli na njia ambazo huzitumia watalii

(f) Kutoa magari ya kuwaongoza (msafara) kwa watalii wanapotaka kutembelea mbuga

(g) Kutoa ushauri wa jumla kwa waongoza watalii na

(h) Kufanya kazi yoyote ambayo itaonekana ina manufaa kwa usalama wa watalii

## 9.3 Uzoefu kwa Nchi ya Uganda

Uganda kwa kutumia Sheria yao ya Utalii[14] na kwa kushirikiana na kitengo maalum cha kulinda Usalama wa Watalii,[15] wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika suala la ulinzi na usalama kwa watalii. Kikosi hicho hutoa msaada kwa kuwalinda watalii na wageni. Polisi hufanya kazi katika sehemu za mahoteli, fukwe na vivutio vyengine vya utalii zikiwemo sehemu za bustani na mbuga. Aidha, Polisi hufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na taasisi inayohusiana na Sekta ya Utalii kwa lengo la kuondosha uhalifu dhidi ya utalii wa ndani na utalii wa nje, ingawa hakuna uhalifu kwa kiwango kikubwa.

Ni jukumu la Serikali kuhakikisha wageni wanaofika Uganda wanabaki kuwa salama na jeshi la utalii nchini humo, kwa kiwango kikubwa sana limechangia kuimarika kwa usalama wa watalii na mali zao. Sanjari na hayo, Uganda ina jeshi maalum la msafara ambalo huwasindikiza watalii wanapokwenda katika

[14] UgandaTourism Act, 2008
[15] Ugand Police Force Unit

maeneo ya wanyama pori (mbugani) ili kufika katika safari zao kwa usalama. Jambo la msingi kwa jeshi la utalii nchini humo ni kulinda uhalifu kutotokea[16].

### 9.4 Uzoefu wa Nchi ya Rwanda

Utalii nchini Rwanda unazingatiwa kuwa ndio msingi mkuu wa kukuza uchumi wa nchi na kuweza kufikia malengo yao waliyojiwekea kwa mujibu wa Dira ya 2020. Kutokana na dhamira hiyo, Serikali imejipangia mikakati imara juu ya muundo wa kuboresha sekta ya utalii nchini humo ikiwemo azma kuu ya kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watalii wanaofika nchini humo[17].

Kwa kuona umuhimu wa ulinzi na usalama kwa watali, Sera[18] imeeleza kwamba Kanuni maalum za kuweka ulinzi na usalama kwa watalii zitatungwa kwa kuweka muongozo mzuri kwa wageni hao.

### 9.5 Uzoefu kwa Nchi ya Madagascar

Katika nchi ya Madgascar, kiwango cha uhalifu kwa watalii kipo chini sana ukilinganisha na nchi nyengine za Afrika. Wengi wanazingatia kwamba visiwa vya Madagascar ni sehemu salama za kutembelea, ingawa kumekuwepo kwa baadhi ya matukio ya kihalifu[19].

Watalii wengi hufika Madagascar kwa kuangalia vivutio vya utalii vya kipekee kama vile kobe, “Flora and Fauna” na venginevyo.

### 9.6 Uzoefu kwa Nchi ya India

Katika nchi ya India, Jeshi la Utalii hufanya kazi katika maeneo maarufu ambayo watalii hutembelea. Kama ilivyo kwa nchi nyengine, mara baada ya

[16]Realmafricansefaris.com Uganda –tourism police
[17] UNWTO-Barametter http:www.unwto.or/facts/eng/barametter .htm
[18] Rwanda Tourism Policy 2009, Kigali - Novemba
[19] David Newsome, Susan A.Moore, Roosk Dowling Natural Area Tourism Ecology Impact Publication p.63

jeshi hilo kuteuliwa, hupatiwa mafunzo ili kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi. Mafunzo hayo hutolewa na kituo cha polisi cha Wilaya. Mafunzo ambayo hupatiwa askari wa kawaida baada ya kuhitimu mafunzo hayo kwa muda wa wiki mbili, hupatiwa mafunzo maalum yanayohusiana na utalii kwa kuwajengea uwezo.[20]

Nchini India, imependekezwa kwamba Polisi wa Utalii wawepo chini ya Serikali ya India kama Polisi wengine, ingawa Wizara ya Utalii ya India itatoa msaada wa kifedha kwa Serikali kwa utekelezaji mzuri wa malipo. Askari hao watapatiwa fursa ya kufanya kazi sehemu za watalii na kuweza kudhibiti uhalifu maeneo ya utalii.

Muongozo utakaotumika katika kufanya kazi zao ni kanuni za polisi wa Wilaya mpaka pale itakavyopendekezwa vyenginevyo. Mkurugenzi wa Idara ya Utalii kwa Serikali husika atakuwa ndio msimamizi wa polisi wa utalii.

Kazi za askari wa kitengo cha Utalii ni kama wanazofanya askari wengine wa kazi hiyo ya kuwalinda watalii na mali zao. Jambo la msingi zaidi ni kuwa askari utalii wa India hufanya kazi pia ya kuwasimamia watalii pale wanapotaka kubadilisha fedha zao "Foreign Currency Exchange" kwa kuhakikisha wanawapeleka katika maduka ya kubadilisha fedha yaliyo halali na benki zilizo rasmi. Aidha, askari hawa pia hufanya kazi ya kuingilia kati ikiwa mtalii atajishirikisha na madawa ya kulevya na kumchukulia hatua muafaka ikiwemo kumkabidhisha kituo cha polisi.

[20] Crime in India 2014-CRB

## 11.0 Mapendekezo.

### 11.1 Mapendekezo ya Kisheria.

- Sheria ya Utalii Nam. 6/2009 ifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 11 kuruhusu kisheria kuanzishwa kwa Jeshi la Utalii ili wazo hilo liweze kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.
- Sheria ieleze wazi kwamba Waziri anaweza kutunga miongozo kuhusiana na kifungu hicho cha 11 cha sheria Nam. 6/2009 kinachoanzisha Jeshi la Utalii.

### 11.2 Mapendekezo ya Kimuundo

(a) Jeshi liundwe na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kamati za ulinzi na usalama za Mikoa

(b) Maafisa wa jeshi hilo wapatiwe mafunzo chini ya Kamisheni ya Utalii kupitia Makamanda wa Mikoa

(c) Taarifa ya utendaji wa jeshi hilo ziwe zinawasilishwa kila wiki kwa Kamisheni na kupelekwa Mkoa.

(d) Uwezeshaji wa kifedha wa maafisa wa jeshi hilo uwe chini ya Vikosi vyao lakini Kamisheni itoe posho maalum kwa ajili ya kufanya kazi kwa muda wa ziada katika kiwango kitakachokubaliwa.

### 11.3 Mapendekezo mengine.

(a) Mara tu baada ya kuanzishwa jeshi la Utalii, vyombo vya habari vitumike kutoa ujumbe kwa wananchi kwa kutumia michezo na

maigizo ili kuwatia hofu wenye dhamira na nia ovu dhidi ya watalii kusitisha dhamira zao.

(b) Kamisheni ya Utalii kutayarisha vipeperushi mbali mbali kusambaza ujumbe na elimu kuhusu madhumuni ya jeshi hilo na umuhimu wake katika utalii na uchumi wa nchi kwa ujumla.

(c) Kuomba ushauri na mashirikiano ya karibu na Jeshi la Polisi ili kuweza kupatiwa mbinu za kuweza kufanikisha majukumu yao.

(d) Kuwashajihisha wananchi kushirikiana na jeshi hilo litakaloanzishwa katika ulinzi kwenye sekta ya utalii

(e) Kutumia mbinu za Kisayansi katika ulinzi katika maeneo ya utalii ikiwemo kufunga kamera za CCTV ili kubaini uhalifu unaokusudiwa kufanywa dhidi ya watalii na kuweza kuukinga usitokee.

(f) Kutengwa kwa fedha za usimamizi wa Jeshi hilo.

## 10.0 Hitimisho

Ulinzi na Usalama ni jambo lisiloepukika kwa nchi yoyote inayotaka kupiga hatua katika kukuza utalii nchini mwake. Takribani nchi nyingi kwa sasa ulimwenguni wamelipa kipaumbele suala hili kwa kuanzisha majeshi maalum kwa ajili ya kusimamia ulinzi na usalama kwa watalii na mali zao. Nchi inaweza kuwa na vivutio vizuri na vya kipekee lakini kama hakuna ulinzi na usalama, hakuna mtalii ambaye atakuja kufurahia mapumziko yake katika nchi hiyo isiyo na amani na utulivu.

Kwa upande wa visiwa vya Zanzibar ni wakati muafaka sasa kuanzisha jeshi maalum ambalo litasimamia suala hili la ulinzi na usalama kwa watalii ili

kukuza sekta ya utalii na kuendana na malengo ya Serikali ya awamu ya nane ya kukuza utalii katika soko la Kitaifa na Kimataifa kwa faida ya vizazi vilivyopo sasa na vinavyokuja baadae.

Kufuatia utafiti uliofanywa na Tume ya kurekebisha sheria kupitia Makala ziliondikwa, Sheria za nchi nyengine na uzoefu kutoka nchi mbali mbali, Tume inashauri kwamba kwa sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha jeshi hili la Utalii visiwani humu, kwa lengo la kuongeza pato la nchi, kuitangaza nchi sambamba na kuunga mkono uboreshaji wa Uchumi wa Bluu kupitia sekta hii ya Utalii.

## (1)USHAURI WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA KUANZISHWA KWA JESHI LA UTALII

**Kuanzishwa kwa Jeshi la Utalii**

Tume ya Kurekebisha Sheria imeona ipo haja ya kuanzishwa jeshi la utalii ambalo litasimamia usalama wa watalii na mali zao. Jeshi hilo lianzishwe kupitia Sheria ya Utalii Nam. 6 ya mwaka 2009.

Tume inashauri jeshi hilo liwe chini ya Kamisheni ya Utalii kwa kuwa litakuwa na mchanganyiko kutoka majeshi mbali mbali hivyo, Kamisheni itaweza kuwaweka wahusika wote katika nafasi moja na kuweza kufanya kazi katika mazingira yanayowiana.

Kifungu cha kuanzisha jeshi hilo inapendekezwa kisomeke kama ifuatavyo:-

*s. 11(1)“Kutakuwa na Jeshi la Utalii ambalo litafanya kazi ya kulinda usalama kwa watalii na mali zao”*

*(2) Kwa madhumuni ya kuondoa hofu kwa watalii, Jeshi la utalii litafanya kazi katika mfumo wa Polisi Jamii.*

*(3) Kamisheni ya Utalii itaongoza utendaji kazi wa Jeshi la Utalii.*

*(4) Waziri ataweka miongozo juu ya uendeshaji wa jeshi hilo.*

**(a)Kazi za Jeshi la Utalii**

Tume inashauri jeshi hili kupangiwa kazi zake maalum kwa ajili ya kusimamia ulinzi na usalama kwa Watalii. Kazi zifuatazo zinapendekezwa kuwa ni miongoni mwa kazi zitakazolazimika kutekelezwa na jeshi hilo kwa mujibu wa Sheria:-

- *(a)Kusimamia watalii pale wanapokwenda katika vituo vya utalii.*
- *(b)Kufanya doria na kuweka ulinzi katika maeneo ya fukwe na vivutio vya utalii.*
- *(c)Kuhakikisha usalama wa watalii wanapokuwa viwanja vya ndege na bandarini;*
- *(d)Kushahijisha na kusimamia waongoza watalii na wenye hoteli kuwapeleka watalii hao katika benki au maduka ya kubadilisha fedha yaliyo rasmi pale watalii wanapohitaji kubadilisha fedha.*
- *(e)Kuhakikisha watalii wanafuata mila, silka na utamaduni pale wanapotoka katika sehemu zao walizofikia.*
- *(f) Kudhibiti matukio yote ya kihalifu yasitokee dhidi ya watalii na mali zao.*
- *(g)Kumkamata na kukamkabidhisha katika kituo cha polisi, mtalii yeyote atakayejishirikisha na dawa za kulevya au biashara nyengine haramu.*
- *(h)Kufanya kazi nyengine yoyote ambayo itapelekea ulinzi na usalama kwa watalii kuimarika.*

**(b) Uongozi wa Jeshi na Muundo wake**

Kufuatia uzoefu wa nchi mbali mbali kuhusiana na jeshi la ulinzi kwa watalii na mali zao, Tume inashauri Jeshi hili lianzishwe kwa kuwashirikisha askari mbali mbali kutoka majeshi tofauti kama vile Askari Polisi, Askari wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Askari wa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), wanajamii na baadhi ya wafanyakazi kutoka Kamisheni ya Utalii. Kifungu kinachoelezea uongozi na muundo wake inapendekezwa kisomeke kama ifuatavyo:-

(3) "*Jeshi la Utalii litaongozwa na Kamisheni na kujumuisha askari kutoka Idara mbali mbali kwa mashirikiano ya wanajamii na wafanyakazi kutoka Kamisheni"*

**(c) Stahiki za Jeshi**

Kuhusu suala la malipo ya jeshi hili na stahiki nyengine zote, kila askari Tume inapendekeza alipwe kupitia jeshi au kikosi chake na Kamisheni itoe posho pale ambapo itaona inastaki kufanya hivyo. Kifungu kinapendekezwa kisomeke kama ifuatavyo:-

*"Wajumbe wa Jeshi la Utalii watalipwa katika taasisi zao husika, na Kamisheni inaweza kulipa posho ama stahiki nyengine pale ambapo itakapohitjika kufanya hivyo"*

**(d) Vyanzo vya Fedha vya Jeshi la Ulinzi**

Tume inapendekeza kwamba kwa ufanisi mzuri na utekelezaji ulio imara kwa jeshi hili, ni vyema kuwa na vyanzo vya fedha ili jeshi liweze kujikimu katika

kufanikisha majukmu yake. Maeneo yafuatayo yanapendekezwa kuwa vyanzo vya fedha.

*"Jeshi litapata fedha kwa kupitia vyanzo vifuatavyo":*

(i) *Kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali;*

(ii) *Kamisheni itapokea kiasi cha asilimia watakaokubaliana baina ya Waziri anayehusika wa Fedha na Waziri wa Utalii katika mapato yanayokusanywa yatokanayo na shughuli za utalii;*

(iii) *Fedha zinazoweza kutolewa kama ni msaada, zawadi au michango kutoka kwa wafadhili wa sekta ya utalii;*

(iv) *Na fedha nyengine yoyote halali itakayoonekana inafaa.*

**(e) Mamlaka ya Waziri katika kutengeneza miongozo**

Tume inashauri Waziri husika wa Utalii awekewe kifungu ambacho kitamtaka atengeneze miongozo kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa Jeshi hilo. Kifungu kinapendekezwa kisomeke kama ifuatavyo:

*"Waziri anaweza kutunga miongozo juu ya mambo yafuatayo:*

*(a) Muongozo wa uvaaji wa sare kwa jeshi la Utalii*

*(b) Muongozo wa kuteua mtu wa kusaidia utendaji kazi katika jeshi*

*(c) Muongozo wa ulipaji wa posho na stahiki kwa jeshi*

*(d) Muongozo wa utendaji kazi wa jeshi na*

*(e) Muongozo mwengine wowote ambao utakuwa na tija kwa utendaji kazi wa jeshi.*